

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS**

Anwani ya Simu: **"TUME"**  
DAR ES SALAAM  
Namba ya Simu:0738166703  
Fax: 255 - 022 – 246011  
Barua pepe:  
[secretary@psc.go.tz](mailto:secretary@psc.go.tz)  
**Tovuti:** [www.psc.go.tz](http://www.psc.go.tz)



TUME YA UTUMISHI WA UMMA,  
6 MTA A WA ALBERT LUTHULI,  
KITALU NAMBA 10,  
S.L.P. 9143,  
**DAR ES SALAAM.**

**MAAFISA UTUMISHI WANATAKIWA KUTEKELEZA MAJUKUMU YAO KWA  
KUZINGATIA SHERIA**

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma, Bw. Nyakimura Muhoji amewaagiza Maafisa Utumishi kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Maelekezo halali yanayotolewa na Serikali wakati wa kushughulikia masuala ya kiutumishi kwa Watumishi wa Umma.

Bw. Muhoji amesema hayo wakati wa kikao cha Wakuu wa Idara za Rasilimali Watu kutoka katika Halmashauri za Chamwino, Dodoma (Jiji), Kongwa, Bahi, Chemba, Kondo DC, Mpwapwa, Kondo TC na Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma pamoja na Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Umma kilichofanyika jijini Dodoma.

Bw. Muhoji amesema Maafisa Utumishi wanatakiwa kutambua kuwa wataalam katika fani zingine wanawategemea Maafisa Utumishi katika kuwashauri masuala mbalimbali yanayohusu Rasilimali watu. Maafisa Utumishi wakilegalega wataalam hao hawatafanya vizuri, watashindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo na kusababisha kutofikiwa kwa malengo ya Taasisi.

Kuhusu mafunzo kwa watumishi wa umma, amesema Maafisa Utumishi wanao wajibu wa kutoa elimu, si kwa watumishi wapya tu, bali pia kwa watumishi wengine wote ili waweze kutekeleza majukumu yao vizuri.

Akizungumzia matumizi ya kusoma nyaraka mbalimbali, Bw. Muhoji amesema kuwa ni muhimu sana Maafisa Utumishi wakarejea nyaraka mbalimbali zinazotolewa na Serikali wakati wa kushughulikia masuala ya watumishi.

Kwa upande wake, Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulikia Miundombinu katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Happiness Mgalula, ameishukuru Tume ya Utumishi wa Umma kwa utekelezaji wa jukumu lake la ukaguzi wa Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma lililofanyika Mkoani Dodoma. Amesema wataendelea kuboresha maeneo yaliyobainika kuwa na upungufu, lengo likiwa ni kuhakikisha usimamizi wa Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma unaimarika.

Imetolewa na:-



Richard M. Cheyo  
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
TUME YA UTUMISHI WA UMMA  
28 FEBRUARI, 2020